

## **9:11-15 MATUMAINI KWA WAKATI UJAO**

Baada ya muda wa hukumu hizo, Amosi anaona msamaha wa Mungu. Kifungo katika nchi ya kigeni kitakomesha mifarakano na mgawanyiko baina ya taifa la Israeli kaskazini na lile la Yuda kusini. Mungu atarudisha taifa litakalokuwa limeunganika tena katika nchi yake watu wake watakapoishi kwa usalama na mafanikio chini ya utawala wa mfalme wa mbari ya Daudi. Utawala wa Israeli utaenea hata katika mataifa mengine yanayoonyeshwa hapa kwa mfano wa Edomu (11-12). Nchi itakuwa na rutuba sana, hata nafaka zitakua na kuiva upesi zaidi kuliko zitakavyoweza kuvunwa. Wavunaji watashindwa kumaliza kazi yao kabla ya msimu mpya wa kupanda tena. Miji itajengwa upya, na wenyeji wake wataishi katika furaha na usalama (13-15).

Baraka zilizoonyeshwa hapa ni kubwa kupita zile za Israeli ya baada ya kifungo. Katika Agano Jipya mfano wa Amosi kuhusu utawala wa mfalme wa mbari ya Daudi juu ya mataifa unahusishwa katika uenezaji wa ufalme wa Kristo katika mataifa yote (Mdo 15:13-18; Efe 3:6). Bila shaka kutakuwa na utimizaji mkubwa zaidi wa maneno hayo wakati ujao (Rum 8:19-23; 1 Kor 15:24-28).